

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA TANESCO

KUTOKA KWA: MWENYEKITI

KWENDA KWA: WENYEVITI WA
WA MATAWI, MAKATIBU,
WAWAKILISHI WA WANACHAMA
NA WANACHAMA WOTE

REF: TS/WALAKA/2013/01

DATE: 20.11.2013

Yah: WASTAAFU WA TANESCO KUENDELEA KUWA WANACHAMA WA TANESCO SACCOS.

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Mkutano Mkuu wa Chama wa mwaka 2013 uliofanyika tarehe 1 had 3 Novemba 2013 Jijini Dar es Salaam, pamoja na mambo mengine, ulipitisha Mpango Mkakati wa Chama kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014 hadi 2018. Katika Mpango Mkakati huo, suala la wastaafu kuendelea kuwa wanachama wa TANESCO SACCOS limepewa kipaumbele.

Nachukua nafasi hii kuwajulisha mambo ya msingi ya kutekeleza wakati utaratibu mzuri wa namna ya kushughulikia kundi hili muhimu la wanachama unaandaliwa:-

- i. Wanachama wanaofikia umri wa kustaafu na ambao wangependa kuendelea kuwa wanachama wasitoe akiba zao kwenye Chama,
- ii. Kwa kuanzia, wanachama waliostaafu na wanaotarajia kustaafu wafungue akaunti na wapitishie pensheni zao katika Benki ya CRDB,
- iii. Wastaafu watakaopenda kuendelea kuwa wanachama na ambao wanapata pensheni zao kupitia Benki ya CRDB waiagize benki kupitia 'standing order' kukata michango yao ya kila mwezi na kuiwasilisha TANESCO SACCOS.
- iv. Wa anuani yako na mawasiliano yako mengine ya uhakika.
- v. Taratibu zingine mtajulishwa mapema iwezekanavyo.

Ni matumaini yangu kuwa uanachama wa TANESCO SACCOS utakuwa uanachama wa kudumu.

K.n.y: TANESCO SACCOS



SOMOE I. NGUHWE